*Nordic Journal of African Studies 16(3): 298–319 (2007)*

# Upekee wa Utenzi wa Swifa ya Nguvumali: Utenzi wa Mpito, Mseto wa Imani za Jadi Na Usasa

MWENDA MUKUTHURIA
*Egerton University, Kenya*

## ABSTRACT

Nguvumali epic is arguably a unique epics amongst the Kiswahili classics. The features that make this epic unique include narration artistry, successful use of dialogue, well-elaborated characters, and classical themes which are relevant to the contemporary society. Nevertheless, this epic has not attracted much attention. In consequence, this paper is a modest attempt to focus on the most basic aspects of any literary work, i.e. theme, character, and language, to explicate its uniqueness and to facilitate understanding of this poem in order to pave the way for further productive criticism. At the end, we have also recommended some of the rich areas which can be explored in the future. It is expected that this paper will contribute to the understanding of Kiswahili classic epics among the young, upcoming critics.

## 1. UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Gerard (1981) utenzi wa Swifa ya Nguvumali ulitiwa katika maandishi miaka ya 1950. Awali, utenzi huu ulikuwa katika hali ya masimulizi. Utenzi wa Swifa Nguvumali unasimulia kisa cha ajabu katika eneo la Kilwa kuhusiana na jinsi mauaji ya mwanamke mmoja yalivyosababishwa na wachawi, ambao baadaye walitambuliwa na mganga maarufu ajulikanaye kama Nguvumali. Utenzi huu ni hazina ya utamaduni wa jamii ya bara ambayo japo ilikuwa imeathiriwa na utamaduni wa Uislamu haikuwa imeachana na imani za uchawi na ushirikina. Maudhui mengine ambayo yanapatikana katika utamaduni huu ni kama vile ya kejeli kwa maongozi ya serikali yasiyofaa, usaliti, umuhimu wa ushirikiano na taasubi za kiume. Kimsingi, masuala haya hayajapitwa na wakati katika utamaduni wa Kiafrika, hasa tukizingatia maongozi yasiyofaa miongoni mwa mataifa huru ya Afrika pamoja na taasubi za kiume ambazo zimekithiri hivi kwamba zinapelekea ubaguzi wa kijinsia ambao unapigwa vita katika jamii ya kisasa inayotetea usawa wa jinsia. Kwa hivyo mambo haya, ambayo hayajapitwa na wakati yanaupa utenzi huu uhalali wa kuzingatiwa katika uchambuzi kama mmojawapo wa tenzi zinazosifika katika Kiswahili.

## 1.1.1 Nguvumali

Nguvumali anayezungumziwa katika utenzi huu ni mhusika aliyeumbwa kisanaa na mtunzi. Hata hivyo, kwa mujibu wa Lienhardt (1968), kulikuwa na Nguvumali wa historia, mganga Mmatumbi aliyekuwa amefunzwa uganga na mngindo aliyeitwa Hamed Matoroka. Huyu Nguvumali wa historia anasemekana kuwa aliheshimika na aliwasaidia watu kwa ukweli wa uhodari wake wa uganga ambao ulifanya visa vya uchawi kupungua Kilwa. Hata hivyo, Katika kumhukumu Nguvumali huyu wa kisanaa, hatujamwegemeza na mhusika mwingine yeyote yule wa kihistoria bali tumemhakiki kwa upekee wake.

## 1.1.2 Mtunzi

Mtunzi wa utenzi huu ni Hasani bin Ismaili (1968) kama inavyodhihirika katika ubeti wa 389. Ubeti huu unatufahamisha kuwa utunzi wake ulianza baada ya mamaye kumpokeza kitabu cha babuye wa kuukeni aliyekuwa mtunzi wa zamani. Kwa hivyo, mamaye Hasani bin Ismaili alipomkabidhi Hasani kitabu hiki kama alivyokuwa ameusiwa na baba yake (babuye Hasani) alikisoma na kikawa ndicho mshawasha uliomfanya kutunga shairi hili. Haya yanapatikana katika beti za 387–389 kama ifuatavyo:

Baada ya kutoka chuoni
Mama akanita ndani
‘Kitabu (h)iki zamani
Baba alikuwekea.’

Nikaona mwanzo wake
Mpaka na mwisho wake
Yote maneno yake
Moyoni yakaniingia.

Hivyo ndio asili
Hasani bin Ismaili
Ikawa mtungaji wa kweli
Bila moja kupotea.

Mambo mengine tunayoyajua kuhusiana na mtunzi huyu ni kuwa mazingira alimotungia utunzi wake ni Kilwa.

## 1.1.3 Asili ya Utenzi wa Swifa ya Nguvumali

Asili ya utenzi huu wa Swifa Nguvumali ni mwambao wa Afrika Mashariki ambao umekaliwa na makabila ya Kibantu ambayo ndiyo asili ya lugha ya Kiswahili. Sehemu hii ya Kilwa hasa imekaliwa na Wamrima. Miongoni wa

makabila haya, imani za uchawi na ushirikina zimetia mizizi sana. Kwa kuzingatia utenzi huu, tunaona kuwa umeshughulikia imani za jamii hizi. Uchawi na ushirikina ni nguvu zinazoaminiwa kuwa si za kawaida. Nguvu hizi zinamilikiwa na baadhi ya watu na wanazitumia kuwaletea wengine madhara. Katika utenzi huu, swala hili linadhihirishwa kuwa lina mizizi yake katika utamaduni na lina suluhisho lake katika jamii. Katika kubainisha jambo hili, msanii wa utenzi amemjenga mhusika Nguvumali kama mtu aliye na uwezo wa kutatua shida hii. Hivyo, anakabiliana na genge la wachawi lililohusika na mauaji ya Salima kwa kuwalisha dawa ambazo hatimaye zinawatambulisha na kuwafanya warogi kama vile Shambi, Binti Jizi, Binti Hanifu kuchukuliwa hatua za kisheria.

Licha ya watu wa jamii hii kuwa na imani na ushirikina wana imani na waganga ambao kazi yao ni kuwahudumia wale ambao wamepatwa na mikasa ya uchawi ili kuwatibu. Waganga kama Nguvumali, pia, nguvu zao si za kawaida; hii ndiyo sababu ujuzi wao huweza kupambana na wachawi. Kwa mfano, baada ya wachawi kusababisha mauaji, Nguvumali aliitwa kusudi kukabiliana nao. Inavyodhihirika kutokana na utenzi huu ni kwamba matendo ya kichawi yanaeleweka katika jamii hii; hii ndiyo sababu Salima anatambulikana kwa urahisi kuwa ameuliwa na wachawi baada ya watu kuchunguza na kuona kuwa alikuwa amekatwa ulimi wake (ub. 240):

Wakamwinua maiti
Wakamuona tofauti
Ulimi kati kwa kati
Wamekata kuchukua.

Kutokana na ujumbe unaopatikana katika ubeti huu, wachawi katika jamii hizi hukata sehemu za viungo vya mwili wa mwanadamu na kuvichukua. Hii ndiyo sababu watu waliweza kubainisha kwa urahisi kuwa mauaji yale yalikuwa yamesababishwa na wachawi.

### 1.1.4 Kiini

Utenzi wa Swifa Nguvumali una kiini chake katika maswala ya kijamii. Unacholenga hasa ni imani za utamaduni wa Mwafrika, hasa imani za uchawi na ushirikina, maongozi dhaifu ya serikali yasiyo na njia mwafaka za kukabiliana na matatizo ya raia, usaliti pamoja na taasubi za kiume. Pia, ushirika unadhihirishwa kama nguzo ya kutatua matatizo.

## 1.2 Yaliyosimuliwa katika Utenzi

Mtunzi wa utenzi huu ametumia usimulizi kutuelezea kisa ambapo wachawi wanne, Bw. Shambi bin Dima, Binti Jizi, Binti Hanifu na Binti Ramadhani wanapokutana katika kilinge na kumwamuru Binti Hanifu kutoa nduguye

mhanga kwa genge hili la wachawi. Bila kuwa na huruma na dadaye, Binti Hanifu anakubali rai hili na kusaidia wachawi wenzake kumshawishi Salima ili waweze kumpata. Hatimaye wanafanikiwa kutekeleza kitendo chao kiovu. Baada ya kitendo hiki Binti Ramadhani anajitenga na wenzake.

Kupotea kwa Salima kunazua wasiwasi na Bw. Mwenye anapeleka ripoti kwa Bw. Hamisi na Liwali, Bw. Nafusi. Katika harakati za wanakijiji kufanya msako mkali wa kutafuta Salima, Bw. Shambi bin Dima anajisaliti pamoja na wenzake kwa kupendekeza kuwa mganga maarufu Nguvumali angeitwa kutatua swala hili. Maoni haya yanakubaliwa bila kusita; hivyo, waraka unaandikwa na wazee wa kijiji ambao unakabidhiwa Yasini Kamina na Hamadi Ramadhani kumpelekea Nguvumali. Hali hii inamtia Shambi wahka; hivyo, anafanya mpango wa kupeleka maiti ya Salima katika kibanda kiovu kusudi wazingizie ndicho kiliporomoka na kumuua.

Jitihada hizi hazikufua dafu; baadaye, mwili wa Salima ulipatikana bandani, ripoti ikapigwa kwa polisi ambao wanakuja kwa fujo ya kuwapiga watu huku wakiwatia washukiwa mbaroni. Kabla ya kuyatekeleza haya yote, Nguvumali alikuwa amefika. Kwa vile mganga huyu alikuwa ameheshimika sana, Liwali anaandika barua kuagiza washukiwa warudishwe ili washughulikiwe na Nguvumali. Kabla ya mganga kuwashughulikia wachawi wote, Binti Ramadhani anaaga dunia. Wachawi waliosalia wananyweshwa dawa na Nguvumali ambazo zingewatia ulevi kubainisha kuwa walishiriki kitendo kiovu cha mauaji ya Salima. Baada ya ithibati hii kupatikana, Nguvumali anawakabidhi kwa Liwali ili wachukuliwe hatua za kisheria. Wanawake Binti Jizi na Binti Ramadhani wanahukumiwa kufungwa miezi mitano kila mmoja huku Shambi akifungwa miezi kenda. Hatimaye, Nguvumali anawanywesha watu wote dawa zake ili kuangamiza wachawi kwa ada ya senti sitini. Baadaye, Binti Hanifu hakujaliwa kukamilisha kifungo chake. Alifariki akiwa jela. Vilevile, Nguvumali aliyekuwa Mganga maarufu alikuwa amekufa kwa ajali ya gari.

Kabla ya kutathmini upekee wa utenzi huu na jinsi ulivyo utenzi wa mpito ulio mseto wa imani za jadi na usasa, katika sehemu zinazofuata, tutapitia maudhui na vipengele vya fani tukizingatia wahusika, muundo na matumizi ya lugha. Hii ni kwa sababu hukumu ya suala hili kwa ujumla itazingatia vipengele vya fani na maudhui.

## 2. Maudhui

### 2.1 Imani za Uchawi na Ushirikina

Katika Utenzi huu, kuna wachawi wanne. Bwana Shambi Bin Dima ambaye ni kinara wa wachawi, Binti Jizi aliyekuwa kiongozi wa wachawi, Binti Ramadhani, na Binti Hanifu ambaye anaagizwa na wachawi wenzake atoe nduguye mhanga kwa wachawi wenzake (ub. 40).

'Binti Hanifu mwambie
(H)apo atoe nduguye
Ao yeye afidie
Sisi tutampokea

Inaaminika kwamba kawaida ya wachawi ni kuwa baada ya muda, huhitaji kafara ambayo aghalabu huwa ni ya mwanadamu. Hivyo, hii ndiyo inayoagizwa na wachawi hawa. Kafara hii ina masharti kwani anayeagizwa kuitoa akishindwa, basi ndiye huifidia kafara ile kwa kupoteza maisha yake kama tunavyoarifiwa katika ubeti wa 40 hapo juu.

Kwa jamii zilizo na imani ya uchawi kama hii, wanaamini kuwa wachawi wana nguvu za kipekee za kuweza kuwatumia watu urogi wakiwa mbali, na hivyo kukamilisha kitendo cha kuroga. Hii inamaanisha kwamba si lazima ujue unaporogwa kwa sababu nguvu za warogi si za kawaida kama inavyoelezewa katika ubeti wa 68:

Binti Hanifu mdogo
Alikwenda kama gogo
Yamemfika marogo
Bila Mwenyewe kuyua.

Pia, wanaamini kuwa dawa wanazozitumia zinaweza kutumiwa kumwita mtu kusudi aende mahala walipo ili wamtende walitakalo. Katika utenzi huu, inadhihirika katika beti 75–76 kwamba ni dawa za waganga ambazo zilimpeleka porini bila kujijua:

Salima Binti Hanifu
Anakwenda bila hofu
Zimempata harufu
Dawa zimemkorea.

Hakika wachawi (h)ao
Wamechapapo dawa zao
Huja wamtakao
Ndivo wanvotumia.

Kutokana na imani hii ya uchawi, mambo yasiyo ya kawaida yalihusishwa na uchawi na ushirikina. Hivyo, kadhia kama ile ya kupotea kwa Salima Binti Hanifu, ambaye hakuonekana baada ya kuchukuliwa na wachawi, ilihitaji mganga wa kuitatua na kuweza kufumbua fumbo hili ambalo mtu wa kawaida asingeweza kulitatua. Ni kwa sababu hii Bw. Shambi, kwa kujifanya kuwa ni mtu mwema, anapendekeza kuwa Nguvumali, mganga maarufu, atafutwe kusudi kufumbua kitendawili hicho. Ubeti wa 185 unaweka wazi pendekezo la Bw. Shambi kuhusiana na jinsi ya kutatua kadhia hii:

'Nguvumali afike
Afanye uganga wake
Na kiumbe aoneke

Mimi ninahitajia.’

Shambi aliyasema haya bila kutilia maanani kuwa yangemponza yakitekelezwa. Kwa hivyo, maneno yake yanamsaliti baadaye kwani wazee wanapokutana wanayatilia maanani na kuamua kuwa Nguvumali aongoze kutatua kadhia hii, hali ambayo inapelekea Shambi kuvumbuliwa kwamba ni mchawi.

Kwa vile itikadi hizi zina mizizi yake katika jamii, watu wanajua wachawi na matendo yao. Watu wanaweza kutofautisha mikasa yenye chanzo chake katika ushirikina; kwa mfano, tunaona kuwa haikuchukua muda kabla ya watu kugundua kuwa kifo cha Salima kilikuwa kimesababishwa na wachawi. Hii ni kwa sababu mwili wake ulipopatikana bandani iligundulikana kuwa haukuwa na ulimi. Kwa hivyo, ilikuwa wazi kuwa kitendo hicho ni cha wachawi kwa kuwa ndio wana tabia ya kukata viungo vya siri vya watu ili kuvitumia katika kufanyizia dawa zao. Kwa mfano katika ubeti wa 240, ugunduzi huu ulielezewa hivi:

Wakamwinua maiti
Wakamwona tofauti
Ulimi kati kwa kati
Wamekata kuchukua

Bwana Hasani Bin Ismaili, katika utenzi wake, anaendelea kutudhihirishia kuwa itikadi hizi si za mtu mmoja; takribani watu wote wameathirika hivi kwamba hata viongozi wa serikali wanategemea matokeo ya imani hizi ili kufikia uamuzi wao. Mfano katika utenzi huu ni pale ambapo Liwali Suleimani Nafusi anapoandika barua ya kuagiza kuwa washukiwa wa mauaji ya Salima waachiliwe na polisi kusudi ‘wapimwe’ na Nguvumali (beti 299–300):

Barua inawasili
Kwa jina la Bwana Liwali
Wachawi wote safari
Kipimo kimewajia.

‘Rudini kwa Nguvumali
Ukapimwe kwa uzuri
Jumla ya watu wale
Mwenginewe kabakia.

Kwa ujumla, utenzi huu umetudhihirishia kuwa uchawi na ushirikina ni vipengele vya utamaduni wa jamii; yaani itikadi iliyo katika utamaduni wa jamii zenye imani hii na inaathiri watu wengi. Hata hivyo, pale ambapo itikadi kama hizi zimeshika mizizi pana hatari ya kutozingatia haki kisheria. Ushahidi unaothibitisha kwamba dosari hii inaweza kutokea unaonekana, kwa mfano, pale ambapo Liwali Nafusi anapoagiza wachawi washukiwa ‘wapimwe’ kwanza na Nguvumali kabla ya kuchukuliwa hatua ya kisheria.

## 2.2 KEJELI

Licha ya kushughulikia imani ya uchawi na ushirikina, utenzi huu umejikita kama kejeli kwa maongozi dhaifu ya serikali yasiyo na njia mwafaka ya kukabiliana na matatizo ya raia. Katika utenzi huu Bw. Mwenye anapopeleka ripoti kwa Jumbe Hamisi, Jumbe hashughulishi polisi katika msako kwa haraka. Hii ndiyo sababu inayowafanya wazee kuamua kwa haraka kuwa Nguvumali angewapatia suluhisho kwa haraka kuhusiana na shida hii iliyowakabili katika kijiji cha Mteniyapa.

Jumbe na Liwali tena wanaonyesha kutoshughulika na shida zilizokuwa zikiwatatiza raia waliokuwa wakiwaongoza na hata kufikia kurudi makwao baada ya msako wa kumtafuta Salima kutofua dafu. Jumbe na Liwali kwa hivyo ni Wahusika waliochorwa kuonyesha mfano wa viongozi legevu waliojaa utepetevu. Hii ni kwa sababu inabainika ni kama kwamba raia wanawashurutisha kufanya kazi, hasa wanapoenda kuwaita kwa mara ya pili mwili wa Salima unapopatikana (ub. 242):

> Palepale ikajili
> Kuitwa tena Liwali
> Na kajumbe wale wale
> Wanje kuhudhuria.

Baada ya Jumbe na Liwali kufika mahala mwili ulipopatikana, walidhihirisha wazi kuwa hawana ushirikiano na polisi. Wao pia, kama raia wa kawaida, walikuwa wanaogopa polisi. Kwa hivyo, walisema kuwa hawawezi kufanya lolote kwa kuchelea hatua itakayochukuliwa na polisi. Woga huu wa Jumbe unabainika katika (ub. 257):

> ‘Ikisikia polisi
> Kwangu mimi ni mkosi’
> Kajibu Jumbe Hamisi
> ‘Kweli! Nakubalia.’

Tamko kama hili ambalo linapatikana katika ubeti huu linadhihirisha ukosefu wa ushirika na kutoaminiana miongoni mwa watawala; Jumbe, Liwali na polisi. Liwali na Jumbe ni kama kwamba hawajui umuhimu wa kuarifu polisi mkasa huu haraka iwezekanavyo. Raia wa kawaida, Bw. Mwenye, ndiye anaonekana kuelewa manufaa ya kuwapigia polisi ripoti kama anavyomwambia Jumbe na Liwali katika ubeti wa 259:

> ‘Liwali na Jumbe Hamisi
> Nitaitaka polisi
> Waje hima kwa upesi
> Tujue la kulijua.’

Ubeti huu unadhihirisha kwa uwazi hali ya kinaya kwani Jumbe na Liwali ndio wanapaswa kuwa na mawazo kama haya lakini siyo raia wa kawaida. Polisi

wanapoitwa kushughulikia tukio hilo, kuwasili kwao katika tukio la kisa hicho kunakuwa kwa fujo nyingi. Hawawaheshimu raia wa kawaida kwa kufanya upelelezi usio na fujo. Wanazua zahama kila pahala bila kuwajali Liwali na Jumbe, ambao ni viongozi wa jamii hiyo. Askari Mnyamwezi na Mjaluo waliwapiga watu wote bila kubagua. Haya yalitokea baada ya Liwali kusimulia polisi yaliyotokea kama inavyoelezwa katika beti za 280–281:

Baada ya kupata hayo
Mnyamwezi na Jaluo
Viliingia vibao
Aibu kusimulia.

Ukipata kofi moja
Kusimama hamna haja
Anakuzusha daraja
Viatu kukushindia

Matendo kama haya ya polisi kupiga raia wasio na hatia hata ikiwa uhalifu umetendeka karibu nao bila shaka ni ya kishenzi, kwani maongozi mema ya serikali yatasisitiza mtindo wa upelelezi usio na fujo na vitisho kwa raia wake. Ithibati nyingine inayoonyesha kuwa serikali hii haikuwa na mwongozo mwema ni kitendo cha Liwali kuagiza washukiwa watolewe mikononi mwa polisi kusudi ‘wapimwe’ na Nguvumali. Kitendo hiki hakifai kwa sababu haimkiniki imani ya watu kupewa kipaumbele kutafuta ushahidi wa kutumika kisheria. Hali hii inaweza kuwa na maonevu kwa wasio na hatia. Kwa mfano, baada ya Bw. Shambi, Binti Hanifu na Binti Jizi kulishwa dawa na Nguvumali, anawahukumu kuwa ndio wenye hatia na kuwakabidhi kwa polisi kama inavyoelezewa katika ubeti wa 351.

‘Ninakupa watu (h)ao
Mnyamwezi na Jaluo
Asikali wenye tao
Ni watu (h)ao chukua.’

Matendo haya yanaonyesha wazi kuwa sheria ya serikali ya nchi hii haihakikishii raia usawa kwa kuwahukumu sawa. Kwa mfano, japo wachawi hawa walikuwa wametenda uhalifu sawa, wanawake walifungwa miezi mitano huku Bw. Shambi akifungwa miezi tisa (ub. 378):

Miezi mitano wanawake
Na Bwana Shambi peke yake
Miezi tisa juu yake
Mkubwa kazidishiwa.

Halafu wanamotiwa kifungoni ili warekebishe tabia, hatimaye mmoja wao Binti Hanifu anafariki. Hali hii yadhihirisha kuwa vituo vya urekebishaji wa tabia za watu haviko katika hali nzuri. Lau vingalikuwa katika hali nzuri, Binti Hanifu hangalifariki akiwa kifungoni. Matatizo haya yote yanazuka kwa ajili ya

maongozi ya serikali yasiyozingatia maslahi ya raia na haki za binadamu; hivyo, mtunzi wa utenzi huu ameutumia kukejeli maongozi ya serikali yasiyofaa.

## 2.3 USALITI

Maudhui ya usaliti pia yamejitokeza katika utenzi huu. Usaliti ni hali ya mtu kutoa habari za uongo ama ukweli kutoka kundi moja hadi lingine kwa ajili ya kuchonganisha wahusika. Ni hali ya kutokuwa na imani na siri fulani na kwa hivyo unaitangaza. Katika utenzi huu, Binti Ramadhani na Binti Jizi wanajitokeza kama wasaliti; naye Bw. Shambi anajisaliti mwenyewe. Kwanza kabisa, Binti Hanifu anasaliti dadaye kwa genge la wachawi kwa kuafikiana na rai za wachawi wenzake kumuua (Salima). Katika kutekeleza kitendo hiki, anashirikiana kwa karibu na Binti Hanifu; hivyo, wote ni wasaliti. Usaliti wa Binti Hanifu pia ndio unamfanya ashiriki katika njama ya kusetiri mauaji ya dadaye kwa kushiriki katika mpango wa kuweka maiti yake ndani ya banda ili ionekane kana kwamba ni banda lililomporomokea na kisha akafa. Aidha, anatoa maelezo yafuatayo anapoutambulisha mwili wa dadaye (ub. 233):

> ‘Nimemwona bandani
> Alikuja vunja kuni
> Kwa nini nimeamini
> Banda limemwangukia.’

Naye Mwana Binti Ramadhani anasaliti kundi lake la wachawi na kutengana nao hali ambayo inawatia wenzake wasiwasi kama inavyobainika katika ubeti wa 129:

> Mwana Binti Ramadhani
> Akajitoa kundini:
> ‘Toka leo abadan
> Siwezi kushuhudia.

Usaliti huu wake unaendelea hadi wakati ambapo anajiunga na watu wema na kuwaongoza katika kutafuta Salima porini alikomwacha na wachawi wenzake. Hata hivyo, jitihada zake zinaambulia patupu kwani anakuta wachawi wenzake wakiwa wamemficha mbali. Haya tunayapata katika beti za 174–175:

> ‘Sasa twendeni twendeni!
> Wanaume jipangeni!’
> Moyo binti Ramadhani
> Alianza kujitia.
>
> Kajitia mbembele
> Kuonyesha kulekule
> Kumbe asumbuka bure
> Wenziwe wamemtoa.

Kwa upande mwingine, Bw. Shambi bin Mdima anaropokwa na maneno ambayo mwishowe yanamponza hasa wakati anapotoa pendekezo kuwa mganga Nguvumali aitwe ili Salima aonekane; maneno haya yanapatikana katika ubeti wa 185:

‘Nguvumali afike
Afanye uganga wake
Na kiumbe aoneke
Mimi ninahitajia.’

Matamshi haya anayatoa kiudanganyifu ili asigunduliwe alikuwa mmoja wa wale waliokuwa na hatia. Hata hivyo, wazee wa kijiji wanayatilia maanani wanapokutana kule Mteniyapa na kumwita Nguvumali ambaye baadaye anamtambua Bw. Shambi akiwa mmoja wa wauaji wa Salima. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa Shambi kwa maneno yake alijisaliti na kujitia mashakani. Hii ni kwa sababu kama sio kutaka kujipendekeza, pengine watu wasingemkumbuka Nguvumali.

## 2.4 UMOJA NI NGUVU

Maudhui mengine yanayopatikana katika utenzi huu ni **umoja ni nguvu**. Ushirikiano umedhihirishwa wazi kuwa ndio njia ya pekee ya kutatua matatizo. Ama kwa hakika, kama asemavyo Shaaban Robert, ‘Matatizo ya watu huondolewa na bidii kuu za watu.’ Mkasa wa kupotea kwa Salima unathibitisha hali ya ushirika wa watu wa jumuiya yake. Bw. Mwenya anajitoa kwenda kupiga ripoti kwa Jumbe na Liwali; pia, ndiye anajaribu kuonyesha Jumbe na Liwali manufaa ya kuwapigia polisi ripoti kuhusiana na kisa hiki.

Ushirikiano wa jamii hii vilevile unajitokeza pale watu kama Shambi wanalazimika kujiunga na shughuli za kumtafuta Salima hata ikiwa alikuwa miongoni mwa wauaji. Lau angejitenga, angejulikana mara moja. Jamii kwa ujumla ilishiriki katika shughuli ya kumtafuta Salima kwa wingi; hivyo, walifanikiwa kupekua sehemu zote kama inavyobainika katika beti za 166 – 167:

Vijana wa mtaani
Hakubakia jelani
Waliyekuwa mashambani
Wote walihudhuria.

Wakubwa wa vijijini
Wengi sita wa a(r)baini
Akina Shambi amini
Na wao walijitia.

Tunaona ushirika zaidi wazee wanapokutana Mteniyapa na kufanya shauri mara moja la kumleta Nguvumali. Vilevile, ushirika unaonekana wakati ambapo vijana Yasini, Amina na Hamadi Ramadhani wanapoitikia mwito wa kuupeleka ujumbe wa kauli ya wazee kwa Nguvumali. Ushirika huu wa watu hawa, ndio unafanya jitihada zao zifanikiwe. Hatimaye, wanafanikiwa kuwatia washukiwa mbaroni hata ikiwa hawakujaliwa kumpata Salima akiwa hai.

Nguvumali naye, akiwa mwanajamii anaonyesha ushirika kwani hakukataa mwito wa dharura. Kinyume na ushirika huu, viongozi wa serikali kama Liwali, Jumbe na askari polisi hawana ushirika; kwa sababu hii, hawana wepesi wa kutekeleza shughuli zao. Kwa hivyo, ushirikiano unaleta umoja ambao dhoruba yake inaweza kupasua mwamba wowote ule.

## 2.5 Taasubi za Kiume

Taasubi za kiume, kwa kiasi, pia zinajitokeza katika utenzi huu. Hizi ni hisia za wanaume kujionyesha kwamba wao ndio bora kuliko wanawake katika shughuli zote. Katika kundi la wachawi, mwanamme (Bw. Shambi) ndiye kinara wa wanawake wote ambao ni wachawi kama vile Binti Hanifu, Binti Jizi na Mwana Binti Ramadhani. Katika kundi hili, shughuli ambayo wanawake wananasibishwa nayo ni ya uchawi isiyo na umuhimu katika jamii; aidha, inadhihirika kuwa wanawake hawawezi kujiendeleza pasipokuwa na wanaume mbele yao. Vilevile, katika harakati za kutafuta Salima, wanawake hawaonekani wakiwa na nafasi kubwa katika shughuli hii muhimu ya jamii. Wanaotekeleza kazi kubwa ni wanaume kama Bw. Mwenye aliyeenda kupiga ripoti, Yasini na Hamadi Ramadhani, vijana waliompelekea Nguvumali risala. Kwa hivyo, katika shughuli ya kumtafuta Salima, wanawake wanatajwa kwa ujumla tu pasipo kupewa wajibu wa kutekeleza. Kwa mfano, katika ubeti wa 160:

> ‘Jamaa wote wafike
> Waume na wanawake
> Na mgeni asibaki
> Kama alipofikia.’

Ubeti huu unawataja wanawake tu; viongozi wa shughuli nzima ni wanaume. Kwa mfano, Jumbe ni Bw. Hamisi, Liwali ni Suleimani Nafusi; wote ni wanaume. Binti Ramadhani, anayesaliti wachawi wenzake na kwenda kuongoza kundi la wanaume kusaka Salima, hafui dafu kwa kazi anayoitekeleza. Mwishoni anaposhindwa anatoa malalamiko kama haya (ub. 181):

> Binti Ramadhani hakika
> Maneno alitamka:
> ‘Wanaume wamenizunguka
> Akili imepotea’

Maneno ya mwanamke huyu ni ishara ya kuvunja mioyo na yanadhihirisha kuwa wanaume ndio walishiriki kwa wingi katika shughuli hii. Nguvumali, mganga maarufu, pia ni mwanamume. Ni muhali kutaja kwamba mambo haya yote katika utenzi huu yanadunisha mwanamke na kukuza utukufu wa mwanamume katika jamii ambayo kisa chake kinasimuliwa katika utenzi huu.

## 3. WAHUSIKA

Katika utenzi huu, masimulizi yamekuza sifa za wahusika kadha ambazo hazina budi kuzingatiwa.

### 3.1 NGUVUMALI

Ni mganga wa kiasili ambaye anawasilishwa na mtunzi kama mtu aliye na sifa sana kwa kuwatambua wachawi pamoja na kutoa uchawi (ub. 294):

> Wamerudi na Nguvumali,
> Mganga wa kiasili,
> Hata chini ya Jibali
> Uchawi anautoa.

Huyu Nguvumali ndiye anawatambua wauaji wa Salima ( ub. 296):

> Kumpa yote habari
> Kasema ‘Sitakubali
> Walete leo kamili
> Wabaya nitawajua

Sifa za mganga huyu maarufu zilikuwa zimetambulikana hata na viongozi wa serikali. Kwa mfano, hata Liwali alimtambua. Kwa hivyo, kutokana na kutambulikana huku, Liwali alimpa kibali cha kutekeleza kazi yake (ub. 303):

> Na wale wakawasili
> Kwa yule Bwana Nguvumali
> Mwenye uganga kamili
> Na serikali inajua

Dawa zake alizowanywesha wachawi ziliwafanya waonekane kama walevi (ub. 319):

> Kaanza kwa wanawake
> Kulisha uganga wake
> Aliye mchawi aoneke
> Kilevi kitamjia.

Baada ya kuwalisha wachawi dawa, yaani Binti Hanifu, Shambi na Binti Jizi, kila mmoja aligharamia kwa kulipa senti sitini. Katika utenzi huu, anajitokeza kama kielelezo cha watu wema wanaosaidia jamii kutatua matatizo yanayoikumba. Mtunzi amemwasilisha kama mhusika mkuu katika utenzi huu.

## 3.2 Bw. Shambi Bin Dima

Bwana Shambi Bin Dima ni kinara wa wachawi. Anautekeleza wadhifa wake bila huruma. Ndiye hasa alimtuma Binti Jizi kushurutisha Binti Hanifu kuua dadaye Salima kama tambiko kwa wachawi. Anajitokeza kama mwongo kwani anakana kuwa yeye si mchawi bali ni mganga wa ngoma na anasingizia kuwa ulimi aliopatikana nao ni wa mbuzi bali si wa mtu (ub. 371). Ndiye alikuwa wa kwanza kuleweshwa na dawa za Nguvumali. Kwa hivyo, katika utenzi huu, amewasilishwa kama kielelezo cha mtu mwovu katika jamii.

## 3.3 Binti Jizi

Katika utenzi huu, Binti Jizi ndiye kiongozi wa wachawi. Ni katili asiye na huruma wala utu katika kutekeleza wajibu wake wa uongozi wa genge la wachawi. Alishiriki kumshurutisha Binti Hanifu kumtoa dadaye mhanga kwa wachawi.

## 3.4 Binti Hanifu

Huyu ni katili mwingine ambaye anasemekana kuwa hana shaka wala hofu (ub. 13). Ni katili aliyekubali rai za wachawi wenzake kuwatolea dadake kama tambiko. Hatimaye anafia jela baada ya hukumu ya kifungo.

## 3.5 Binti Ramadhani

Binti Ramadhani ni mwanagenge la wachawi ambaye hana siri anayoificha. Yeye ni kigeugeu kwani hatimaye anawasaliti wachawi wenzake. Ni kielelezo cha watu katika jamii wasio na msimamo na ambao wanaweza kuhiari kufanya chochote iwapo hatima yao iko hatarini.

## 3.6 Binti Salima

Maskini Binti Salima ndiye alitolewa kafara na dadaye, Binti Hanifu, na kuuawa na wachawi. Usaliti huu ulipokuwa ukitokea, yeye hakuweza kung'amua chochote huku akiandamana na dada yake. Katika utenzi huu, amechorwa kama kielelezo cha wanajamii wasio na hatia ambao mara kwa mara huangukia mitego ya watu waovu katika jamii.

## 3.7 Jumbe Hamisi na Liwali Suleimani

Hawa wawili wamechorwa kama viongozi ambao wanatakiwa kuwa karibu na umma katika harakati za utawala. Kimsingi, wanatakiwa kuwa kiungo cha kati baina ya raia na utawala wa juu katika kutatua matatizo ya wananchi. Hata hivyo, matendo yao ni ithibati ya viongozi wasioshughulika na maslahi ya raia, watawaliwa, katika mfumo wa uongozi ulio na utepetevu. Kwa hivyo, mtunzi amewachora kama viongozi wa umma wasiowajibika.

## 3.8 Bandira na Bw. Komera

Hawa wamesawiriwa kama majirani wema wanaowajali wenzao wakati wa dhiki. Kutokana na wema wao, walihudhuria makiwa kwa kina Binti Hanifu ili kuwaliwaza kutokana na msiba uliokuwa umewasibu.

## 3.9 Yasini Kamina na Hamadi Ramadhani

Hawa wamechorwa kama kizazi cha vijana walio na ari ya kusaidia kutatua matatizo yanayokumba jamii yao. Yasini na Hamadi ndio wanaompelekea Nguvumali ujumbe kwa haraka iwezekanavyo ili ufumbuzi kuhusiana na kifo cha Salima upatikane (ub. 165). Ni waaminifu; hivyo, ni kielelezo cha watu wema wanaojitolea kutoa huduma fulani inapohitajika katika jamii.

## 3.10 Kagendu

Huyu alikuwa kinara wa kikao cha wazee wa kijiji waliokutana Mteniyapa na kuamua kumwita Nguvumali. Ndiye aliyetia sahihi waraka uliopelekewa Nguvumali. Yeye ni kielelezo cha watu wema katika jamii wanaojitolea kutatua matatizo ya jamii pale ambapo pana kutowajibika miongoni mwa viongozi wanaostahili kuwa wanaongoza jamii.

# 4. MUUNDO

Utenzi huu una jumla ya beti 393. Kila ubeti una mishororo minne, mbinu ambayo inatumiwa na bahari maarufu ya shairi. Utenzi huu umeasi kaida moja kuu ya utunzi wa tenzi nayo ni kaida ya kina cha bahari.

Alichokusudia mtunzi wa utenzi huu ni kuwa na 'a' kama kina cha bahari. Lakini, kina hiki hakiwiani, katika takribani beti 32 kutoka kwa jumla ya beti 393 za utenzi wote. Hali hii inaufanya utenzi huu kutokuwa na ukamilifu kwa mtazamo wa kimapokeo ukilinganishwa na tenzi za kale. Hivyo, washairi wapenzi wa kaida za kimapokeo watauona kama utungo ulio na sifa ya uguni. Beti zifuatazo zimekiuka kanuni hii: 11, 17, 22, 27, 49, 59, 61, 64, 71, 111, 143, 154, 158, 179, 200, 214, 216, 221, 241, 266, 274, 275, 276, 298, 326, 339, 349, 362, 393. Akizungumzia hali hii, Prof. M. H. Abdulaziz (katika Gerard, 1981: 146) anasema kwamba mtunzi ana mtindo wa kukiuka kaida za urari katika sehemu nyingi za utenzi huu. Anaonelea kwamba mtindo wa namna hii ni wa kimakusudi unaodhamiriwa kuoana na mdundo wakati wa kukariri utenzi huu. Sababu nyingine ambayo anakisia ndiyo chanzo cha ukiushi huu ni hali ya mtunzi kutaka kudumisha maana na ujumbe badala ya kukazania kaida za urari na kupoteza ujumbe wa shairi. Gerard (mtaje: 146) anamnukulu mshairi huyu akisema kwamba:

> Miongoni mwa washairi wa Tanzania ukiushi wa kaida wa namna hii ni jambo la kawaida na hii ni hatua kubwa ya kuepusha ushairi wa Kiswahili na utegemezi mkubwa wa kaida za urari ambazo baadhi ya wahakiki wanahisi kwamba ni udhaifu. *(tafsiri yangu)*.

Hoja hii ni ushahidi kwamba tunapouhakiki utenzi huu, tuziegemee arudhi na kusahau fani na maudhui ambayo yanauweka katika daraja ya kipekee ya tungo za Kiswahili. Misingi inayokaribiana na hii ilitumiwa na Gibbe (1994: 258) kuamua kwamba tungo zote za Abdulazizi Y. Lodhi zina hadhi zote za tungo nzuri.

Pia utenzi huu umetohoa maneno ya kigeni, hasa kutokana na lugha ya Kiingereza, hali ambayo si kawaida katika tenzi za zamani. Kwa mfano ub. 377, neno 'jajimenti' limetoholewa kutoka kwa neno la Kiingereza 'judgement'. Utohozi huu unaubainisha utenzi huu kama mfano wa tungo za kisasa kwani tungo za zamani zilifungwa kwa kutumia lugha ya zamani ya Kiswahili. Athari za kigeni zilizopatikana katika tenzi hizo zilitokana na lugha ya Kiarabu ambayo hati zake ilikuwa neema iliyozihifadhi. Katika beti zingine, utenzi huu hautimizi idadi ya mizani nane ambayo mtunzi alikuwa amekusudia kutumia; kwa mfano, ubeti wa 23 mshororo wa kwanza na wa pili una mizani 7, ubeti wa 82 mshororo wa pili una mizani 6; ubeti wa 201 mshororo wa kwanza una mizani 10, ubeti wa 367 mshororo wa pili una mizani 7. Beti zingine zina mishororo mitatu tu; kwa mfano, ubeti wa 330, 342, na 354. Hali hizi zinafanya utenzi huu kutotimiza arudhi zifaazo za tenzi za kimapokeo. Hata hivyo, utenzi huu

umejaribu kuzingatia tenzi za zamani ambazo zilikuwa zikitanguliza kwa kumtukuza mwenyezi Mungu. Kwa mfano, utenzi huu umeanza hivi:

Bisimillahi naanza
Juna la mola wa enza
Muhammadi mpendeza
Kwa Mola wetu Jalia

Pia tamati ya utungo wake inayomtukuza mwenyezi Mungu inapatikana katika ubeti wa 390 ambapo anahitimisha hivi:

Muniombee kwa Bwana
Mola wetu Maulana
Ya Rabbi ya Maulana
Aninusuru baria.

## 5. MATUMIZI YA LUGHA

Lugha iliyotumiwa katika utenzi huu ni ya moja kwa moja isiyo na mafumbo mengi. Katika utenzi huu pana matumizi ya jazanda. Hii ni hali ambapo neno hupewa maana nyingine isiyo ile ya asilia; mfano, neno 'ngoma' ubeti wa 37 na 'ngozi' ubeti wa 36 yametumiwa kijazanda kumaanisha 'kitu cha kuchezea' vilevile 'ngozi ubeti wa 354 limetumiwa likiwa na maana sambamba na hiyo. Jazanda nyingine ambayo imetumika katika utenzi huu ni ile ya neno 'watu' ubeti wa 351 kumaanisha wahalifu. Ubeti wa 272 una jazanda:

Usiku wa alfajiri
Ikaja mvua ya kweli
Hapapa kujisetiri
Walapo kukimbilia

Mvua hii iliyonyeshea watu usiku ni jazanda iliyoashiria mateso ambayo yangewasibu waliomuua Salima. Pia, 'mvua' hapa ni taashira ya tukio la mateso.

Katika utenzi huu, kuna matumizi ya tashbiha. Hizi ni semi za mlinganisho. Katika ubeti wa 68 mshororo wa pili, tashbiha hii inapatikana: 'Alikwenda kama gogo' - kumaanisha kuwa namna alivyokuwa akienda hakuwa akijijua wala kujitambua. Tashbiha nyingine ni 'Mji unatikisika kama wingu la mvua' (ub. 277); 'Wanaluka kula kama jiwa' (ub. 276); na nyingine nyingi. Vilevile, mafumbo yapo katika utenzi huu. Mafumbo ni hali ya kutumia semi zenye maana fiche kwa mfano katika ubeti wa 373, ' Nguvumali… kujao kunipaka vumbi', kumaanisha kuwa Nguvumali alikuwa anataka kumharibia jina lake. Ubeti wa 186, 'kumbe khadithi ya pweza makaa kujiparia', kumaanisha hali ya mtu kujichumia janga mwenyewe. Ubeti wa 125, tuna fumbo la aina ya methali, 'maji yakimwagika hayazoleki kama taka', kumaanisha kuwa jambo likishaharibika si rahisi kulirekebisha. Matumizi ya usemi wa tanakuzi

yanapatikana. Tanakuzi ni usemi wenye ukinzano wa maana. Kwa mfano, ubeti wa 360, 'ukitaka usipotaka'. Takriri ipo kwa wingi. Takriri neno imetumika kwa mfano katika ubeti wa 92, 'kusemasema sema' ubeti wa 289, neno 'hima' limekaririwa hivi, 'hima hima twene hima'. Hali hizi za takriri zinafanikisha mdundo wa shairi hili.

Kuna matumizi ya mbinu ya tabdila; hapa sentensi inaparaganywa na kuchukua muundo usiofuata kanuni za kisarufi lakini ikiwa inabakisha maana ileile; mfano ubeti 292, 'kwa yao yale mashaka', badala ya, 'kwa mashaka yale yao'. Aina nyingine ya tabdila ni pale ambapo neno linabadilisha sauti moja, lakini bila kubadilisha maana; mfano ubeti wa 1 ambapo neno 'Juna' linatumiwa badala ya 'Jina', 'u' ikiwa imechukua mahala pa 'i'. Kuna mtindo wa kurefusha maneno (mbinu ya mazda) ambapo neno linaongezewa sauti ama silabi lakini bila kubadilisha maana yake. Kwa mfano neno 'molana' badala ya neno la kawaida 'Mola' (ubeti 205). Vilevile, neno 'shairina' ni kurefushwa kwa neno 'shairi'; ubeti wa 17 tuna neno 'tunadharawiya' badala ya 'tunadharau'. Pamoja na mazda, inkisari imetumika pia; yaani kufupisha maneno kwa kuyadondoa silabi ama sauti. Kwa mfano, 'atayechukia' badala ya neno 'atakayechukia' katika ubeti wa 169.

Lahaja ya kimrima, inayozungumzwa Kilwa imetumika katika shairi hili. Pia kuna jitihada za kutumia lahaja ya kaskazini, hasa lahaja maarufu ya Kiamu, ambapo sauti [y] inatumiwa badala ya [ɟ] ya Kiswahili Sanifu. Hivyo, tunapata maneno kama vile 'moya' badala ya 'moja', 'wanayua' badala ya 'wanajua'. Kwa hivyo, katika utunzi wake, mtunzi ameathirika na Kiamu; vilevile, isisahaulike kwamba utenzi wake umezingatia mtindo wa kutumia mistari minne katika kila ubeti, ambao unasadikika kwamba matumizi yake yalianza Lamu. Aidha, katika kujinasibisha na lahaja za kaskazini ambazo zina historia ndefu ya utunzi wa mashairi, maneno ya asili ya lahaja ya Kimvita yanapatikana katika utenzi huu; kwa mfano neno 'matungu' badala ya 'machungu' ubeti wa 81. Ni lahaja ya Kimvita ambayo inatumia sauti /t/ badala ya /ʧ(ch)/. Matumizi ya lahaja ya Kilwa pia yamethibitishwa na Gerard (1981: 146) anaposema kwamba utenzi huu umetumia lahaja ya Kilwa na kwa kiasi ukiwa umetumia msamiati wa lahaja za kaskazini hasa msamiati na baadhi ya vipengele vya kisarufi vilivyotumiwa sana na watunzi wa tenzi bulibuli za kale.

Matumizi ya nidaa yanapatikana katika shairi hili. Nidaa ni semi za msisitizo wa mawazo ama maneno fulani ya mhusika katika kazi ya sanaa ya maandishi. Aghalabu msisitizo huu hutambulishwa katika maandishi na alama ya mshangao (!) kwa mfano, katika ubeti wa 174 maneno 'sasa twendeni twendeni! wanaume jipangeni!' katika mshororo wa kwanza na wa pili katika ubeti huu ni ya msisitizo wa namna hii. Kuna pia mbinu ya usemi halisi ambayo imetumiwa na mtunzi kwa wingi. Mbinu hii imefanikisha fani ya usemezano ambayo imepatia utenzi huu mtindo wa tamthilia unaofanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwa kiwango cha juu cha usanii. Matumizi ya usemi halisi yanahusu hali ya kunakili kile ambacho kilisemwa na mhusika mwenyewe kwa mfano: ubeti wa 21 kuna mfano huu wa usemi halisi: **Binti Hanifu katamka: 'Ni kweli hiyo hakika**

**lakini kuna mashakka mwenewe kuyatambua'**. Huu ni mfano mmojawapo wa semi halisi ambazo mwandishi amezitumia. Kuna nyingi nyinginezo ambazo ziko katika utenzi huu. Kwa kutumia semi halisi, anatujengea sifa za wahusika na kustawisha mbinu ya usemezano katika utenzi wake, ambayo huhitaji ustadi mkubwa sana pale ambapo shairi la ngonjera halitumiwi. Matumizi ya semi halisi yanaandamana na ubadilishanaji wa nafsi mara kwa mara miongoni mwa wahusika hali inayomfanya mtunzi kufanikiwa katika kusawiri mielekeo ya wahusika wake kwa uwazi na kumpelekea kufanikiwa kuwasilisha ujumbe wake kwa mtindo wa drama.

Taashira pia zimetumika katika utenzi huu. Kwa mfano, ubeti wa 210 'nyoka wawili' wanaashiria mabaya yaliyokuwa karibu kumfika bwana Shambi. Kuna utohozi wa msamiati; kwa mfano, neno 'jajimenti' ubeti wa 377 limetoholewa na kutumiwa. Limetokana na neno la Kiingereza 'Judgement'. Kutohoa hasa ni kuchukua neno la kigeni na kuliingiza katika msamiati wa lugha ya Kiswahili ama lugha yoyote ile kwa kulifanyia marekebisho ili liweze kufaa mtindo wa maneno ya lugha pokezi.

Fani nyingine ambayo imedhihirika katika utenzi huu ni ile ya njozi ambayo imetumiwa kudokezea yatakayojiri baadaye. Kwa mfano, ubeti wa 121, Binti Ramadhani anaelezea haya kuhusiana na ndoto yake:

'Kulala ni kibuhuti
(H)ujiona sarakati
(h)ujiotea, mauti
Watu wanichukua

Haya yalikuwa maono yatakayomjiri baadaye kupitia kwa ndoto. Hatimaye Binti Ramadhani aliugua na kufariki akiwa hospitalini. Katika ubeti wa 219, Shambi naye anaota akipewa dawa na Nguvumali. Haya pia yalimpata baadaye Nguvumali alipowanywesha dawa katika harakati za kuwatambua wachawi.

Katika ubeti wa 276, matumizi ya chuku yamejitokeza katika utenzi huu. Chuku ni hali ambapo maelezo yanatiliwa chumvi kwa minajili ya kusisimua ama kuelezea hali fulani, kama inavyojitokeza katika ubeti huu:

Polisi (h)ao wawili
Kama kumi na mbili
Walipanda baiskeli
Wanaluka kama jiwa.

Aidha, maelezo yenye kinaya yanapatikana katika utenzi huu ambapo Bw. Mwenye anasisitiza kuwa angependa polisi waje wajue la kufanya katika ubeti wa 259:

'Liwali na Jumbe Hamisi
Nitaitaka polisi
Waje ima kwa upesi
Tujue la kulijua.'

Tukichukulia kuwa Liwali na Jumbe ndio wanapaswa kuwa na mawazo kama hayo ya huyu raia wa kawaida, hali kinaya inajidhihirisha. Hii ni kwa sababu Jumbe na Liwali, ambao ni viongozi wa serikali, hawaoni umuhimu wa kuita polisi huku Bw. Mwenya akitaka waitwe ilhali yeye si mtawala ama kiongozi.

Kwa ujumla, mtunzi wa utenzi huu ametumia msamiati ambao una urahisi kueleweka. Hali hii inafanya ujumbe wake kufahamika kwa urahisi na kuupa utenzi huu nguvu kimawasiliano. Hata hivyo, ni muhali kutaja kwamba pana uwezekano mtindo huu ukafasiriwa kama udhaifu unaopunguza hadhi ya utenzi huu. Mbinu ya pekee na ambayo ameitumia kwa ustadi mkubwa ni mbinu ya usimulizi wa moja kwa moja. Mbinu hii ikichunguzwa kwa undani, inabainika kwamba ametumia viwango vifuatavyo vya usimulizi:

- Usimulizi-maizi: ambapo anaonyesha ujuzi wa kujua kisa chake kwa undani na kutambua matukio. Katika usimulizi wa aina hii, mwandishi (msimulizi ana uwezo wa kuingia katika nafsi na kutambua mawazo. Kwa mfano, pale ambapo anatumia semi halisi kutusaidia kufahamu hisia za wahusika wake na misukumo ya wahusika hawa. Ueledi wa matumizi ya aina hii ya masimulizi unadhihirika zaidi pale ambapo mtunzi huyu, anatuonyesha sifa kiunguungu katika masimulizi yake anapotumia njozi/ndoto kutabiri yale yatakayojiri siku za baadaye. Hali hii inamdhihirisha kama mtambuzi wa kila kitu katika usimulizi huu. Kwa hivyo, katika usimulizi wake, ametumia viwango vikuu vya usimulizi maizi; yaani usimulizi horomo ambao ni wa kuripoti matukio kupitia njia ya kidrama bila kutumia maneno yake binafsi au kutoa uamuzi juu ya tukio. Aidha, usimulizi dokezi wa kutuelezea mambo na hata sababu yake na kutujulisha yale yatakayotokea.
- Kiwango cha pili cha usimulizi ambacho kimetumika ni cha usimulizi-tinde (*limited narrator*) ambapo tunaona kuwa wahusika wakuu na wadogo katika utenzi wake wanatumiwa kuendeleza usimulizi. Viwango hivi amevidhibiti barabara na kwa jinsi hiyo vimefanikisha uwasilishaji wa ujumbe na uelewa wa wahusika.

## 6. UPEKEE, MSETO WA JADI NA USASA

Utenzi wa Swifa ya Nguvumali una upekee ambao unautofautisha na tenzi za zamani. Suala hili linadhihirika kwa uwazi vipengele vya kimsingi, fani na maudhui, vinapohakikiwa. Japo utenzi huu umelanda tenzi za zamani, lengo na maudhui yake yana upekee. Maudhui hasa yamelenga mseto wa mila za jadi za Waafrika na usasa, hasa wa mifumo ya uongozi mbao nchi za Afrika zimerithi kutokana na ukoloni. Kwa jinsi hii, maudhui haya yameweka utenzi huu katika kiwango cha tungo ambazo haziwezi kupitwa na wakati. Ukiushi wa kaida za mizani, idadi ya mishororo katika kila ubeti na kuasi uwiano wa kina cha bahari ni mtindo ambao unapatia utenzi huu upekee unaoutofautisha na tenzi za kale. Japo umeasi kaida za tenzi kuu za zamani, umefanikiwa katika upande wa fani

na maudhui jambo ambalo ni la kimsingi katika kazi ya sanaa ya maandishi yoyote ile (Gibbe, 1994; Njogu na Chimerah, 1999). Hapana shaka katika karne hii ya 22, mgogoro wa ushairi ushaamuliwa; hivyo ingefaa utenzi huu uchukuliwe kwa hadhi zote za tungo nzuri za Kiswahili. Kielelezo cha tungo ambazo zina sifa sawa na utenzi huu wa *Swifa ya Nguvumali* ni kama vile tungo za Abdulazizi Y. Lodhi za *Utenzi wa Ghuweni* na *Tafkira* (taz. Gibbe, 1994: 258). Akizungumzia tungo hizi, Gibbe (mtaje) anakiri kwamba ni mashairi yasiyozingatia kanuni za utunzi sawasawa; hivyo, hayakuwa yakiheshimika sana na wanamapokeo, hasa tungo za diwani ya *Tafkira* zilizokuwa na vina, mishororo na mizani zilizokuwa zikihitilafiana katika urari. Hata hivyo, amezihakiki na kuamua kwamba zinastahili heshima zote za tungo nzuri kwa sababu riha ya ushairi iko wazi katika tungo hizi kwa mwenye akili tambuzi (Gibbe, 1994: 258). Kauli hii ni dhihirisho kwamba utungo, uwe wa kimapokeo, huru, ama uwe guni kama mashairi ya Abdulaziz Y. Lodhi, una dhima yake katika jamii. Kwa hivyo, hapana haja ya kuzua migawo miongoni mwa mashairi ya Kiswahili. Kwa hivyo, si ajabu kwamba hii leo uhakiki wa ubora wa tungo unalenga fani na maudhui, masuala ambayo yamefanya tungo huru za Kiswahili kukubalika na kuvutia wasomi maarufu wa Kiswahili kote duniani. Vilevile katika utenzi huu, lugha nyepesi inayoafikiana na lugha ya tenzi za kale imetumiwa. Hata hivyo, tofauti na lugha ya tenzi za kale, mafumbo yaliyotumiwa na mwandishi hayana uzito; hivyo, yanaeleweka kwa urahisi kinyume na hali ilivyo katika baadhi ya tenzi za kale kama vile Hamziyya. Upekee mwingine wa utenzi huu umejikita katika fani ya usimulizi ambayo imetumika tangu mwanzo hadi mwisho. Katika kufanikisha usimulizi wake, mtunzi ametumia mbinu ya usemezano kwa ustadi mkubwa. Mbinu hii imefanikisha ujenzi wa wahusika na kuwapa uhalisia, hali ambayo ni nadra kupatikana katika tenzi ama ushairi kwa ujumla. Usemezano pia umepelekea ubadilishaji wa nafsi hali ambayo inafanikisha usawiri wa mielekeo ya wahusika na kuwafanya waeleweke kikamilifu na wasomaji. Usimulizi umesukwa kwa ustadi wa hali ya juu. Kutokana na utenzi huu, aina mbili za usimulizi zimejitokeza ambazo ni usimulizi-maizi na usimulizi-tinde. Ni muhali kutaja hapa kwamba mbinu ya usimulizi ni ya jadi na ina asili yake katika simulizi za Kiafrika ambazo zina ukale kuliko fasihi andishi. Kwa hivyo, matumizi ya fani hii yanaweza kufasiriwa kama athari za fasihi simulizi katika fasihi andishi ama jitihada za mtunzi za kunasibisha kazi yake ya sanaa ya maandishi na mtindo wa sanaa ya jadi hali inayompa upekee usio na kifani.

Zaidi ya haya, wahusika wamejitokeza kwa uwazi kabisa kuliko tungo zingine za aina hii. Ama kwa hakika, wahusika wa utenzi huu wamekuzwa hadi sifa zao zikababinika tofauti na tenzi za zamani ambazo hazijatumia wahusika kwa mapana. Mahusiano ya wahusika hawa yamefanikishwa kwa usimulizi wa kina kuhusiana na sifa zao na kwa kutumia mbinu ya usemezano. Hivyo, wahusika hawa wamejitokeza kwa uwazi kama ilivyo katika fani za tamthilia na riwaya ambazo zina wahusika waliojengwa kikamilifu.

Matumizi ya lugha katika utenzi huu pia yanadhihirisha mtindo wa kuchanganya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Ushahidi wa hali hii ni

utohozi wa maneno kadha ya Kiingereza. Mtindo huu una upekee kwa vile tenzi zote zilizotangulia hazikuwa na matumizi ya lugha ya Kiingereza yaliyokithiri. Tenzi kama vile utenzi wa Hamziyya, na Inkishafi zilitumia Kiswahili. Pia, kwa vile ziliandikwa kabla ya kukita kwa ukoloni wa kimagharibi katika mwambao wa Afrika Mashariki, athari za kigeni zinazopatikana katika tungo hizi zimetokana na lugha ya Kiarabu ambayo wenyeji wake walikuwa na uhusiano wa muda mrefu na upwa wa Afrika ya Mashariki. Jambo lingine linalobainika ni kwamba utenzi wa Nguvumali umetumia kwa kiwango kikubwa Kiswahili sanifu tofauti na Kiswahili cha lahaja kilichotumika katika tenzi za kale. Mtindo huu ni ithibati kwamba utenzi huu ni wa kisasa na ambao unashughulikia hali halisia ya maisha ya jamii za Afrika Mashariki.

Kuhusiana na usasa, ni muhali kutaja kwamba unadhihirishwa na kutozingatia kaida za utunzi ambazo zilitiwa maanani sana na watunzi wa zamani (kimapokeo). Lugha nyepesi inayolingana na ya ushairi wa kisasa imesaidia kufanikisha ujumbe kufahamika. Vilevile, ujumbe ambao unazungumziwa una uhalisi wa utamaduni wa Mwafrika na imani zake za jadi. Aidha, unahusiana na usasa kwa mfano maongozi yasiyofaa ya serikali zenye misingi ya kikoloni. Haya yote, pamoja na ushirikiano unaodhihirika na taasubi za kiume, yamesukwa kikamilifu na kujikita kwa uwazi katika utenzi huu.

Kwa ujumla, mambo haya yote si kawaida ya tenzi za kale wala yote hayawezi kuwekwa katika jopo la sanaa ya ushairi wa kisasa. Kwa hivyo, yanaufanya utenzi huu kuwa wa mpito. Kwa mfano, maudhui yanalenga usasa na imani za ushirikina za jadi. Katika sehemu ya 2.2 ya makala hii, aina mbili za uongozi zinajitokeza. Japo tunawategemea Liwali na Jumbe kuwa viongozi wa mifumo ya kisasa, ya serikali, lakini tunawaona wakizidiwa na imani za jadi za kuwaamini waganga kutoa hukumu badala ya kuwapeleka washukiwa mahakamani; kwa mfano, wanaposhikilia kwamba washukiwa wa ushirikina 'wapimwe' na Nguvumali. Kwa hivyo, hapa inadhihirika kwamba viongozi wanatafuta haki kwa kutumia njia za zamani na za kisasa. Hii inamaanisha kuwa japo ni viongozi wa kisasa, lakini hawajaondokana na imani za jadi. Vilevile mseto wa jadi na usasa unadhihirika kaida za utunzi wa tenzi za kimapokeo zinapotumiwa katika utenzi huu na hali kadhalika ukiushi wa kaida hizo, hali ambayo imekithiri katika ushairi wa kisasa (linganisha na 4.0).

## 7. Hitimisho na Mapendekezo

Makala hii imeshughulikia Utenzi wa Swifa ya Nguvumali kwa kutilia masuala kadha wa kadha maanani ili kuweza kubainisha upekee wa utenzi huu. Kwanza, uvulivuli kuhusiana na mhusika mkuu Nguvumali anayejikita katika utenzi huu umewekwa wazi kwa kumzingatia kama mhusika aliyejengwa na kukuzwa kisanaa. Mambo mengine yaliyoshughulikiwa ni kufafanua asili ya utenzi, kudhihirisha lengo, maudhui na matumizi ya lugha. Mambo haya

yamezingatiwa ili kufanikisha tathmini ya upekee wa utenzi huu na jinsi ulivyo wa mpito unaochanganya mambo ya zamani na usasa.

Kutokana na haya yote, tunapendekeza kwamba utenzi huu ufanyiwe uchunguzi wa jinsi fani ya usimulizi imefanikishwa na mtunzi katika utenzi huu. Aidha, uchunguzi wa kulinganisha utenzi huu na tenzi za kale unaweza kufanywa ili uweze kueleweka zaidi. Katika kufanya hivi, pengine swali ambalo linaweza kutiliwa maanani ni hili: Je, utenzi huu unaingia katika mkondo wa mashairi ambayo yameathiriwa na utenzi wa zamani kama vile inkishafi? Swali kama hili ni muhimu na litapelekea udadisi zaidi kuhusiana na fani na maudhui ya utenzi huu ikizingatiwa kwamba Utenzi wa Swifa ya Nguvumali haupo miongoni mwa tenzi ambazo Gibbe (1994) ameziweka katika jopo la tungo zilizoathiriwa na inkishafi. Kwa jinsi hii, mchango mkubwa utakuwa umetolewa katika fasihi linganishi.

## MAREJELEO


Abedi, A.K.1954.
*Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Gerard, Albert. 1981.
*African Language Literatures: An Introduction to the Literary History of Sub-Saharan Africa*. Burntmill Harlow: Longman.

Gibbe, A.G. 1994.
*Inkishafi*: *Uhakiki wa Kidayakronia.* Tasnifu ya Uzamifu [isiyochapishwa]. Chuo Kikuu cha Moi.

Hasani bin Ismaili. 1968.
*The Medicine Man: Swifa ya Nguvumali*. Peter Lienhardt (Ed. tr.). Oxford.

Knappert, J. 1979.
*Four Centuries of Swahili Verse*. Nairobi: Heinemann.

Mnyapala, M. 1965.
*Waadhi wa Ushairi*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Njogu, K. na Chimerah, R. 1999.
*Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.



**About the Author**: *Dr. Mwenda Mukuthuria* (B.ED, Moi University; M.A., Ph.D, Egerton University, Kenya) is currently a Kiswahili Lecturer at Egerton University, Kenya. He has taught Kiswahili at the Islamic University in Uganda (IUIU) and at the Makerere University in Uganda. His area of interest is Kiswahili Linguistics as well as Comparative and Applied Linguistics. He is a member of the National Association of Kiswahili – Kenya (CHAKITA) and the Kiswahili Association of East Africa (CHAKAMA).